



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آتَيْنَا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَأْتِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَخْلُقُونَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُخْكِنَنَّهُمْ دِيْنُهُمُ الَّذِي أَرْضَى فَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَوْفِهِمْ أَمْانٌ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Toleo: 1445/05 H

Jumatatu, 6 Rabi' II 1445 H

30/10/2023 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Hizb ut Tahrir Kenya yafanya Maandamano baridi kutoa mwito kwa Majeshi ya Kiislamu
Wakomboe Al-Aqsa kutoka kwa Makucha ya Umbile la Kiyahudi

(Imetafsiriwa)

Kufuatia mauaji ya halaiki yanayoendelea kufanya na serikali ya kinyama ya kizayuni dhidi ya watu wa Ghaza, Hizb ut Tahrir Kenya iliweza kufanya maandamano baridi mnamo siku ya Ijumaa Oktoba 20,2023 katika miji ya Nairobi na Mombasa sambamba na miji mengine ya pwani.

Awali, Hizb ilikuwa imepanga kuongoza swala ya Ijumaa kwenye uwanja maarufu wa Makadara Jijini Mombasa kusimama pamoja na ndugu zao wa Palestina, hata hivyo kufuatia hali mbaya ya hewa amali hiyo ikahamishiwa msikiti wa Taqwa. Na baada ya swala ya Ijumaa, maandamano hayo yakafanywa nje ya msikiti ambapo mwito ulielekezwa kwa majeshi ya nchi za Kiislamu hususan Misri, Lebanon na Jordan yaweze kuvunja vizuizi walivyowekewa na watawala wao katika kambi zao ili waweze kunusuru operesheni ya Tufani ya Al-Aqsa kukomboa Msikiti uliobarikiwa wa Al-Aqsa kutoka kwa makucha ya walowezi wa Kiyahudi. Maandamano hayo yalitamatika kwa kufanya mkao mfupi na wanahabari kuangazia mashambulizi ya umbile la Kiyahudi dhidi ya watu wa Palestina.

Hizb ilikariri kwamba majeshi ya Kiislamu na watu wenye nguvu wana jukumu kubwa la kuunga mkono vijana wa Ardhi Iliobarikiwa. Umma wa Kiislamu aidha, ukakumbushwa jukumu lao tukufu la kubeba ulinganizi wa kuregesha maisha ya Kiislamu kwa kuititia kusimamisha Dola ya Khilafah ambayo ndiyo itakayosukuma kikweli jeshi kupambana na dola ya kizayuni na zile zinazoiunga mkono ambazo ni Amerika na Uingereza.

[وَإِنْ اسْتَصْرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ]

“Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini basi ni juu yenu kuwasaidia.” [Al-Anfal 8:72].

Shabani Mwalimu

Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya